**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Tano – Tarehe 22 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo**:

Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

27. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha uongozi wa shehia ilikuwa na mpango wa kuwaajiri makatibu wa sheha badala ya utaratibu wa sasa ambapo makatibu hao huwa wanateuliwa na sheha husika.

(a) Je, ni nani ambaye kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa anatakiwa kuteua katibu wa sheha.

(b) Yapo malalamiko kwa masheha wa zamani ambao wameteuliwa tena kwamba hawakulipwa mkono wa shukrani kabla ya uteuzi mpya kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, Je, suala hili lina ukweli wowote.

29. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya awamu ya saba kwa kipindi kirefu ilijitahidi kuzuia magari ya ng'ombe kuzagaa katika miji jambo ambalo limeonekana kushamiri katika kipindi hiki.

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani ili kuendelea kudhibiti hali hiyo.

(b) Ni hatua gani za kisheria zinazochukuliwa kwa wale wanaobainika kukiuka agizo hilo.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

5. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato kupitia taasisi binafsi ambazo zinatoa huduma zake za kibiashara hapa Zanzibar. Huduma hizo ni pamoja na za chakula na bidhaa mbali mbali zinazotolewa katika majengo ya 'super market' na mikahawa iliyopo hapa Zanzibar.

(a) Kwa kuwa 'super market' na mikahawa mingi hapa Zanzibar haitoi risiti za mauzo, Je, ni utaratibu gani wa kukusanya mapato ya Serikali unaotumika kupitia 'super market' na mikahawa hiyo.

(b) Je, Serikali yetu imewaruhusu wafanyabiashara wa 'super market' na mikahawa iliyopo Zanzibar kutotoa risiti za mauzo ambazo zinatumika kukusanyia mapato.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

135. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Pamoja na nia ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha vijana wanakulia katika maadili mema ya jamii yetu, kumekuwa na malalamiko kwamba hakuna mikakati wala sheria madhubuti zinazotekelezeka wala adhabu stahiki za kuwadhibiti watoto ili waweze kuelekea kwenye maadili sahihi kama vile ruhusa ya

mikato ya nywele inayofaa, miongozo ya mavazi sahihi, na katazo la mimba za utotoni na kabla ya ndoa.

(a) Je, kwa nini adhabu za sasa zinawabagua vijana wa kike na wa kiume, kama vile kumlipisha faini kijana wa kiume pindi vijana wawili wakitenda kosa linalofanana.

(b) Je, ni upi mpango bora wa sasa wa Serikali katika elimu na malezi mema ya vijana, sambamba na maadili mema ya Mzanzibari.

(c) Je, ni lini Serikali itafanya mapitio ya sheria zinazowabana zaidi vijana wa kiume na kuwapendelea vijana wa kike katika makosa yanayofanana.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

72. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Hospitali ya Mnazi Mmoja huwa na utaratibu wa kuwahudumia wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi ya kisukari kwa kuwapima hali zao pamoja na kuwapa dawa na kuwachoma sindano za Insulin. Changamoto iliyopo ni kuwa sindano hizi zimegundulika kuisha muda wake na bado zinaendelea kutolewa kwa wagonjwa jambo ambalo linazidi kuhatarisha afya zao.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea dawa hizi za Insulin kukaa muda mrefu hadi kuharibika.

(b) Je, ni sababu zipi zinazopelekea dawa hizi kuendelea kutolewa na kuwapa wagonjwa wa kisukari wakati tayari zimeshamaliza muda wa matumizi yake.

(c) Je, kuna utaratibu wa kuzichunguza dawa ili kubaini mwisho wa matumizi yake kabla ya kupatiwa wagonjwa.

122. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa filam za x-ray katika hospitali zote za Pemba jambo ambalo linasitisha huduma hii takriban miezi minne sasa ambapo wagonjwa wa moyo hushindwa kupatiwa huduma. Hii ni kutokana na kuwa mashine za x-ray zinazotumia filam ni za kizamani jambo ambalo upatikanaji wake ni shida.

(a) Je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha huduma ya x-ray inapatikana kwa wananchi wa Pemba.

(b) Je, Wizara ina mkakati gani wa kupeleka mashine za kisasa ili kwenda na mabadiliko ya dunia katika upatikanaji wa huduma ya afya.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

12. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na kero ya muda mrefu kwa vilabu vya soka Zanzibar kupata mgao mdogo sana wa fedha zinazotokana na viingilio vya uwanjani kunakosababishwa na utitiri wa makato baada ya makusanyo.

(a) Je, kuna makato ya aina ngapi ambayo fedha hizo huwekezwa kabla ya vilabu husika kupata kasma yake.

(b) Ni nani anayehusika kukusanya na kugawa fedha hizo na kwa utaratibu upi.

(c) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja sasa kuzifuta kabisa kodi hizo ili kuwa na uendeshaji bora wa mchezo huo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

56. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika Serikali ya awamu ya saba kulikuwa na mpango wa ujenzi wa viwanja vya ndege vidogo vitatu (Air-Strips) Kigunda, Paje na Mwambe Pemba, viwanja ambavyo vilitegemewa kuwa ni vya kusaidia marubani kutua kwa dharura iwapo viwanja vikubwa kumetokea dharura yoyote au pia kutumika kwa ajili ya ndege ndogo ndogo hasa kwa huduma za kitalii. Katika utekelezaji kimeweza kujengwa kiwanja kimoja tu hadi sasa na pia kimeachwa hakijakamilika hadi sasa.

(a) Je, lile wazo la kuendeleza ujenzi wa viwanja vile bado lipo.

(b) Na kama lipo, hivi sasa kuna programu gani inayoendelea katika kuendeleza ujenzi wa viwanja hivyo.

(c) Je, Waziri unaweza kutuambia ujenzi wa viwanja hivyo umepangiwa bajeti yake na Serikali au utajengwa na Mamlaka yenyewe ya Viwanja vya Ndege.

116. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ina mpango wa kujenga barabara za ndani zenye urefu wa kilomita mia mbili na ishirini (220).

(a) Je, majimbo mangapi ambayo yatafaidika na mradi huu.

(b) Je, mradi huu utachukuwa miaka mingapi.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

106. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha Kampuni yake ya Uvuvi ya "ZAFICO" ikiwa ni pamoja na kuipatia vifaa vya kisasa ikiwemo meli za uvuvi.

(a) Je, Serikali kupitia kampuni hii ilipanga kununua meli ngapi za uvuvi.

(b) Je, mpaka sasa meli ngapi tayari zimeshapatikana.

(c) Kwa kiasi gani matokeo ya awali ya Kampuni ya ZAFICO yanaonesha kuwa kampuni hiyo ina tija kwenye pato la Taifa.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

155. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wakati wa kuanzisha kilimo cha mpira katika shehia ya Maziwani, Serikali ilichukuwa mashamba kutoka kwa wazee wengi wa jimbo la Pandani na majimbo mengine kwa ahadi kwamba kutajengwa kiwanda japo kidogo kitakachochakata

mpira huo na kuzalisha. Bahati mbaya, hadi sasa ahadi hiyo bado haijatekelezwa.

(a) Je, ni faida gani wamiliki hao wa zamani wa mashamba wamepata.

(b) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga kiwanda japo kidogo ndani ya shehia ya Maziwani.

(c) Je, Serikali ina rasilimali na madeni gani yanayotokana na kilimo cha mpira katika shehia ya Maziwani.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

120. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kuna ukakasi kwa Wizara husika kuwapatia kiwanja wananchi wa Shakani – Buyu kwa lengo la kujenga skuli ili kuondosha changamoto ya wanafunzi wa shehia hizo kufuata huduma ya elimu kwa masafa ya zaidi ya kilomita nne. Kadhia hiyo inapelekea kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji sambamba na ufaulu hafifu kutokana na machofu kwa wanafunzi hao wakati wa kwenda na kurudi skuli kutokana na umbali huo.

Je, ni lini wanafunzi hao watapatiwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa skuli hiyo.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:**

Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**22 Februari, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**